

Seizures First Aid (Swahili)

Msaada wa kwanza kwa degedege

Mshtuko, mtukutiko au degedege (mtetemeko usiodhibitiwa) kwa watoto unaweza kusababishwa na homa, majeraha ya kichwa, kifafa na hali zingine.



Ishara ya degedege



Mkanganyiko



Ugumu au kutetemeka kwa mikono na miguu



Kupoteza ufahamu (kuzimia)



Macho yakirudi nyuma
Kichwa kinarudi nyuma



Kupumua kwa shida

Piga simu kwenye Sifuri Mara Tatu (000) mara tu degedege inapoanza.

Utunzaji wakati wa degedege



Fanya

- umsogeze mtoto wako mahali salama kwenye sakafu/ardhi na ondoa vitu vyenye ncha kali ambavyo vinaweza kumdhuru
- kaa na mtoto wako
- andika wakati mshtuko huanza na kile kinachotokea kwa mtoto wako wakati wa kuanguka ghafla ili uweze kuwaambia maofisa wa ambulensi na madaktari.



Usifanye

- usimshike mtoto wako
- usimwache mtoto wako peke yake
- usiweke chochote katika mdomo wa mtoto wako
- usimpe mtoto wako chakula au kinywaji chochote.

Mara moja baada ya mshtuko

- Pindua mtoto wako kwa upande wake
- Zungumza na mtoto wako kwa utulivu hadi apone kabisa, au usaidizi ufike.

Unaweza kujifunza zaidi kuhusu kumtunza mtoto ambaye ana degedege kwa kukamilisha kozi ya huduma ya kwanza.

Imeandaliwa na Idara ya Dharura, Hospitali ya Watoto ya Queensland. Tunatambua mchango wa watumiaji na walezi. **Resource ID:** FS212
Reviewed: July 2022 **Kanusho:** Maelezo haya yametolewa na wataalamu wa afya kama mwongozo pekee na yanalenga kusaidia, si kubadili nafasi, majadiliano na daktari wa mtoto wako au wataalamu wa afya. Taarifa husasishwa kila mara, kwa hivyo tafadhali angalia kuwa una rejelea toleo la hivi majuzi zaidi. Tafuta ushauri wa matibabu, inapofaa, kwa wasiwasi kuhusu afya ya mtoto wako.

